THE LUTHERAN WORLD FEDERATION

A Communion of Churches

lutheranworld.org

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA

Sermon in Kiswahili delivered by Bishop Dr Fredrick Onael Shoo on 8 October 2017 to mark 500 years of Reformation

MAHUBIRI *Wagalatia 3: 10 - 12*

(THE SERMON TEXT: ***Galatians*** *3: 10 – 12)*

Tumekusanyika hapa ili kudhihirisha umoja wetu na pia kuungana na wakristo wenzetu wa Kilutheri kote duniani ambao wanaadhimisha miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa. Miaka 500 siyo muda mfupi. Napenda kuwashukuru nyie ndugu zangu wote mlioweza kufika.

Neno kuu la kilele cha maadhimisho haya yaliyoanza na Warsha jana 7 Oktoba 2017 ni: "Tunaokolewa kwa neema ya Mungu" na mada ndogo tatu: "Wokovu si wa kuuza," "Wanadamu sio bidhaa ya kuuzwa" na "Uumbaji sio wa kuuzwa."

Tunaokolewa kwa neema. Tunatunzika kwa neema ya Mungu. Tumeona katika kuadhimisha hii miaka 500 tukumbushane mambo haya kwa sababu nyakati zetu kumezuka mitindo mingi na mbinu mbalimbali za wanadamu kujipatia fedha kwa kuwafanya wanadamu wenzao watumwa kwa kufanya biashara hata kwa vile vitu ambavyo Mungu amewapa watu wake bure kwa upendo wake. Sasa wapo watu walioaminishwa kuwa hata wokovu huu ambao Mungu pekee amelipa katika Yesu eti unaweza ukanunuliwa kwa fedha.

Ndugu zangu, watu wanaacha kweli ya Injili. Wanaacha kufurahia uhuru huu wa kweli tunaopewa na Yesu Kristo. Wanaacha kukumbatia uhuru huu. Kwa kujua mimi ni mwanakondoo kundini mwa Yesu; Yesu alikwishaniweka huru. Badala yake tunarudishwa nyuma katika kumkumbatia tena utumwa. Katika Injili ya Yohana, Yesu mwenyewe anasema ukiishafahamu kweli na kweli itawaweka huru. Na mwana akiwaweka huru mnakuwa huru kweli kweli.

Tunapoadhimisha miaka hii 500, ndugu zangu, tunaadhimisha uhuru tuliofunguliwa kutoka minyororo ile. Na uhuru huu Martin Luther alionesha ndio ukweli uliopo katika Neno, kwamba ni kwa neema ya Mungu katika imani katika Yesu Kristo ambaye alimtoa Yeye ambaye alijitoa na nafasi yake ili sisi tuwekwe huru. Mbona tunarudi katika utumwa? Neno tulilosoma toka waraka wa Wagalatia ni miongoni mwa vifungu vilivyomfanya Martin Luther akaanzisha matengenezo ya kanisa katika karne ya 16.

Haikuwa lengo la Dkt. Martin Luther kuondoka katika Kanisa Katoliki wakati ule. Yeye alitaka kanisa lisimame katika ukweli wa Neno la Mungu kuhusiana hasa na suala la wokovu yaani kuhusu jambo la mwanadamu kuhesabiwa haki. Alitaka kuelewa napataje kuhesabiwa haki na Mungu? Napatataje kuhesabiwa haki na Mungu mimi mwenye dhambi. Je ni kwa matendo yangu kwa kufanya jambo la kumpendeza Mungu? Je naweza kweli kulipa adhabu ile ambayo nastahili kama mwenye dhambi?

Martin Luther aligundua kwamba kuna ukweli unaotuweka huru bali si kwa matendo yetu. Si kwa nguvu zetu tunapata kuwekwa huru. Jambo la kusamehewa dhambi, jambo la kuokolewa ni jambo la neema kwa kuamini katika kile ambacho Yesu alifanya pale msalabani. Ndugu zangu hili ndio kiini cha Injili. Huu ndio msingi wa matengenezo ya Kanisa. Wokovu unaopatikana kwa neema na kwa njia ya imani kwa kumwamini Yesu peke yake.

Mwanadamu anayemwamini Yesu anapata msamaha na anaokoka hata kabla ya kutenda jema lolote, wala hajatambua upendo wowote moyoni. Pengine anachokisikia moyoni ni hukumu na mauti, na hicho ndicho kitu kilimwondolea Luther amani moyoni. Akahangaika kwa maombi, akahangaika sana kufanya mambo mengi yaliyodaiwa na Kanisa kwa wakati ule hadi pale Mungu alipomfunulia kwamba kuhangaika kwako ni bure. Akamfunua macho aweze kuelewa alichofanya Yesu pale msalabani.

Jambo la kuokoka na kuokolewa ndugu zangu ni kwa ajili ya Kristo pekee. Bwana Yesu asifiwe. Huu ndio ukweli kuhusu wokovu wetu. Ndio ukweli wa Neno la Mungu na sisi tunasimamia hilo. Tunaposema na kuwaambia wengine kwamba tukae katika Neno la Mungu linavyotufundisha na kubaki katika ukweli wake.

Kuna upotoshaji wa Neno la Mungu, upotoshaji wa Injili ambayo ni Habari Njema inayotuambia mwanadamu wewe mwambie Yesu kwa imani kutokana na kazi yake aliyofanya pale msalabani. Kuna upotoshaji unaotafuta kumwondoa mtu katika Yesu na kazi yake ya ukombozi aliyoifanya msalabani. Na badala yake kukaza kwamba kile alichokifanya Yesu pale msalabani hakitoshi bali lazima na mimi niongezee kitu kidogo. Lakini sivyo ilivyo kwa jambo la wokovu wetu.

Hata leo hii tunaona upotoshaji huo ambapo watu wanarudishwa katika utumwa wakidhani kuwa wanaweza kujinunulia neema ya Mungu kwa kutenda matendo mema au kuongeza vitu; lakini huu ni upotoshaji. Tumefika hatua ya kufanya mambo ya ushirikina kwa kukubali vitu kama hirizi tukifikiri kwamba vitatupatia neema ya Mungu; lakini Neno tulilosoma litukumbushe kwamba haya hayajaanza leo. Mambo ya kupotosha ukweli wa Injili inayowaweka watu huru hayakuanza leo.

Hata wakati wa Mtume Paulo kule Galatia, walijitokeza watu waliofundisha kwamba mtu ataokoka tu kama anatimiza sheria kama ilivyo katika Torati kwa kuwataka watimize sheria yote. Ndipo Mtume Paulo, katika Wagalatia (mimi napenda sana waraka huu wa Wagalatia, waraka huu ulimtia nguvu sana Martin Luther) mlango wa kwanza, anakemea kwa ukali akisema ninashangaa maana mmemwacha upesi hivi Yeye aliyewaita katika neema ya Kristo na kugeukia Injili ya namna nyingine. Wala si nyingine tu bali wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza Injili ya Kristo. Lakini na ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hiyo uliyowahubiri na alaaniwe. Huyu ni Mtume Paulo. Anawastaajabu na kuwashangaa watu wa Galatia watu ambao wamekwisha kumpokea Yesu ndipo pale katika mlango wa tatu anaweka lile swali. Anawaambia enyi Wagalatia msio na akili, ni nani aliywewaloga? Ninyi ambao Kristo aliweka wazi mbele ya macho yenu yakuwaamesulubiwa, nani amewaloga. Ndugu zangu, kama leo Mtume Paulo angekuja atazame KKKT, aingie katika ibada zetu asikilize mahubiri yanayotolewa na awaangalie baadhi ya washarika kwa jinsi wanavyo hangaika huku na huko: Ataona watu wenye mahangaiko kutoka kwa mtumishi mmoja au nabii mmoja hadi kwa nabii mwingine na wanaokwenda hata kwa waganga wa kienyeji.

Mtume Paulo angefika katika Kanisa letu leo sijui kama hili swali angeacha kutuuliza. “Enyi Walutheri ni ni nani amewaloga?” Kwenye baadhi ya sharika zetu unajiuliza nini kimetokea? Nani amewaloga? Nani amekwambia njia za ibada yenu haina utukufu, haina upako? Nani amwewaambia? Mbona hiyo imani mmeondokana nayo? Mbona ndio imani wazazi wenu waliikulia wakabarikiwa sana. Ni nini kinachowahangaisha? Sijui kama leo angeuliza maswali haya. Nimesema wakati wa Wagalatia kulikuwa na hali hiyo na sasa iko hivyo hivyo.

Na wakati wa Martin Luther hali hii ilijitokeza kwa nguvu watu wakadanganywa kwamba wangeweza kusamehewa dhambi zake kwa kujinunulia vyeti vya msamaha. Na vyeti hivi viliuzwa na makasisi, mapadre na kiongozi wao alikuwa ni padre mmoja aliyeitwa Johana Tetzel. Eti kwamba ili Mungu akusamehe dhambi lazima ununue cheti na hivyo vyeti vilikuwa na bei tofauti tofauti kulingana na dhambi zako. Kanisa likakusanya pesa kwa kuuza msamaha wa Mungu unaotolewa bure.

Lakini wakati ule wa Martin Luther jambo hili lilivuka mpaka kwa kusema haitoshi tu wewe mwenyewe kujinunulia cheti ili usamehewe, bali eti hata ndugu yako aliyefariki hata bila toba. Yaani mtu aliyekufa katika madhambi yake eti unaweza kumnunulia cheti cha msamaha. Na hivyo viliuzwa ghali kweli kweli. Mnaona upotoshaji huo. Kwamba mkimnunulia mtu aliyekufa kwenye dhambi huko aliko toharani atafunguliwa, atasamehewa dhambi zake atawekwa huru. Huo ni upotoshaji.

Ndipo Martin Luther akaweka mkazo katika mambo yale ambayo ni msingi wa wokovu hata kwetu sisi wa leo. Neno tu, neema tu, Kristo tu, imani tu. Tena akakaza kwamba tunaokolewa kwa neema. Tunawekwa huru . Mwisho akasema ni kwa utukufu wa Mungu pekee asije mtu akajisifu. Asije mtu

akajiona ni bora kuliko wengine. Maana siku hizi kuna watu wanaondoka na kuwa na vikundi vyao wakidhani kikundi chao sijui kilichopo kwenye Kanisa lao au chini ya mtumishi fulani ndio eti kina upako kuliko vingine. Halafu mahali pengine watu wamefika mahali wanapotangaza Ibada hizo na mikutano hiyo, siyo tena Yesu wala msalaba wake unaoinuliwa, bali kinachoinuliwa ni picha ya mtumishi husika. Watu wamefika mahali ambapo wameondoa imani yao na utii wao kwa Yesu. Anayetetemekewa na kuabudiwa ni mwanadamu yule ambaye anayeitwa mtumishi. Tunakwenda wapi?

Neno la leo ndugu zangu, linatuasa tusidanganyike wala tusidanganywe kwamba kuna njia nyingine ya kupata wokovu isipokuwa kwa njia ya imani. Ibrahimu aliye baba wa imani ni mfano wa kweli. Yeye aliamini katika ahadi ya Mungu kwamba Ibrahimu hatuambii alifanya nini kabla lakini alimwambia Ibrahimu nimekuteua wewe, nimekubariki wewe na uzao wako na wewe utakuwa baraka kwa mataifa. Ondoka toka katika nchi ya baba yako na mimi nitakuonyesha mahali utakapo enda. Kilichofuata ni Ibrahimu kuitikia tu kwa imani kwamba kwa ahadi hii yeye Mungu amefanya tena katika Yesu Kristo kwa kuweka ukombozi pale msalabani. Ametuambia aminini katika hili. Katika hili nitawasamehe dhambi zenu. Muamini kwamba Yesu amewalipia deni lenu. Mwaminini yeye.

Lakini angalia tunamwamini hivyo? Tunategemea kwamba wokovu wangu, usalama wangu ni pale kwenye msalaba wa Yesu? Amini utii. Ibrahimu akatii akaenda kama vile Mungu alivyoagiza. Hebu watu wa Mungu turejee katika hilo. Msalaba wa Yesu unatosha. Kazi ya Yesu msalabani inatosha. Ninamwamini huyu. Namtegemea huyu. Hakuna kitu kinachochangia katika wokovu unaotolewa na Mungu ni kwa neema yake tu. Huu ni uhuru tunaitwa kumwamini huyu Yesu. Ukimtegemea mpaka kufa utapata wokovu.

Na mtunzi wa wimbo "Mwamba wangu wa kale" anaosema mkononi sina kitu ila msalaba wako. Mimi ni mtupu nipe nguo. Mimi ni mnyonge nipe nguvu. Niondolee dhambi, niondolee takataka zangu nitakase ee, Bwana Yesu kabla sijafa. Hiyo ndio imani ya Kilutheri. Tunaitwa kurejea katika jambo hili la msingi. Tusidanganywe na wababaishaji wanaofanya biashara ya kutuuzia maji kutoka Nchi Takatifu eti, oo sijui kama wapo miongoni mwa watu walionunua maji. Eti ili biashara ibarikiwe. Oo sijui watoto wafaulu masomo, upate mchumba, mume sijui awe nini? Mbona tunadanganywa? Maji toka nchi takatifu, mafuta kutoka Nigeria. Ni Walutheri wanaonunua vitu hivyo kwa bei ghali sana. Sasa kazi ya Yesu pale msalabani ilikua ni nini?

Narudia tena: Mimi ni mwanakondoo kundini mwa Yesu aliyenifia msalabani ninatunzwa vizuri na huyu Mchungaji wangu mwema. Anayenipenda kabisa. Amini katika hilo. Nasema: mafuta, maji au chumvi ndugu zangu vitu hivi haviongezi chochote katika wokovu wetu. Ndio ujumbe tunaoambiwa. Tunaambiwa mwenye haki ataishi kwa imani wala si kwa matendo mema maana hatuwezi kutimiza madai ya torati. Hatuwezi kwa kipimo cha Mungu na utakatifu wake. Je, wewe ni nani unayeweza kusema kwa matendo yangu mema basi mimi mbele za Mungu naweza kujipiga kifua kwamba nastahili? Hakuna. Omba ufunikwe na neema hii. Ufunikwe na kazi ya Yesu pale msalabani. Aliikamilisha kazi ya kutukomboa. Hadai kitu kwako zaidi ya kumpokea Yeye kwa imani na Yeye atakupokea jinsi ulivyo. Na baada ya hapo ndipo anaposema kuwa kwa njia ya imani tunapokea ahadi ya roho. Ukishampokea huyu Yesu Yeye anatupa Roho ambaye anatuongoza na kutuwezesha kuishi maisha ya kumzalia Mungu matunda mema.

Ukisoma pale katika ule mlango wa tano anasema: “Ni kweli ninyi ndugu mliitwa mpate uhuru, lakini uhuru wenu isiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tutumikianeni kwa upendo. Hiyo ndio kazi ya Roho Mtakatifu anafanya katika wale wanaomwamini Yesu Kristo. Tumewekwa huru lakini ni uhuru wa kumtii baba na Yeye Roho Mtakatifu ndiye anayetuwezesha. Roho ya unyenyekevu na ya toba ndio njia ndugu yangu ya kupokea neema hii ya wokovu tuliyopewa bure kwa njia ya Kristo. Yeye akituweka huru tunakuwa huru kweli kweli. Hutuwi tena watumwa wa ibilisi. Hatuishi tena katika hofu ya mapepo, uchawi na kulogwa.

Watoto nyie mnaogopa eti sijui mtalogwa. Eti kule shule kuna kitu kinaitwa misukule au vibwengo. Yuko rafiki yangu alitoka Dar es Salaam alitaka nimtafutie shule tukapata shule nzuri ya masista. Kukaa kidogo, mara naona mtoto anarudishwa pale nyumbani. Nini mtoto? Aa kule ni vibwengo vinanisumbua. Jamani watu wa Mungu, watoto wangu wapendwa, nawaombeni muamini katika ulinzi wa Yesu. Yesu ndiye anayekulinda. Usikae katika hofu.

Shetani anatumia hofu kututeka, kutuondoa katika imani. Nawaombeni isiwe hivyo. Kristo akituweka huru ndani yake, tunakuwa huru. Na huu ndio mkazo wa matengenezo ya Kanisa. Tunaokolewa kwa neema kwa njia ya imani katika huyu Yesu kristo. Hivyo nakuomba hilo tuendelee kutangaza hili tuwaambie na wengine kuwa tunaokolewa kwa neema kwa njia ya Yesu Kristo peke yake. A